JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU

| | | |
|---|---|---|
| Tell: 2533015 au 2533016<br>Fax: 027-2533016<br>Email: md@mbuludc.go.tz<br>Mbulu-Manyara | MBULU DISTRICT COUNCIL | Mkurugenzi Mtendaji (W)<br>S.L.P 74<br>MBULU. |

**TANGAZO LA KOTESHENI YA UKUSANYAJI WA ADA YA TAKA NGUMU NA UZOAJI WA TAKA NGUMU KWA KIPINDI CHA KUANZIA AGOSTI 2023 HADI JUNI 2024**

TAREHE: **29/06/2023**

Halmashauri ya wilaya Mbulu katika Mwaka wa Fedha **2023/2024** inakusudia kutoa ***KAZI YA UKUSANYAJI WA ADA YA TAKA NGUMU NA UZOAJI WA TAKA NGUMU KWA KIPINDI CHA KUANZIA AGOSTI 2023 HADI JUNI 2024*** katika miji midogo ya Dongobesh, Maghang na Haydom kuanzia mwezi Agosti 2023 hadi mwezi Juni 2024. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu anawatangazia wananchi, makampuni na Taasisi mbalimbali kuleta maombi ya Utoaji wa huduma hiyo.

**MASHARTI YA KUOMBA KOTESHENI ZA UWAKALA WA MAPATO**

1. Koteheni inapatikana kwa kulipa ada ya shilingi 50,000 (Elfu hamsini tu) kwa kila koteshent. Nyaraka za kotesheni zinapatikana kwenye ofisi ya Manunuzi na Ugavi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu.
2. Zingatia kuwa fomu ya maombi ya kotesheni inajazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (Power of Attorney) katika kotesheni hii.
3. Mwombaji wa kotesheni endapo atachaguliwa, atalazimika kuilipa Halmashauri fedha taslimu Tsh. 10,000,000/= (Milioni kumi Tu) ambayo ni dhamana ya kazi anayopewa kabla ya kuanza kazi. **Mshindi wa kotesheni hataruhusiwa kuanza kazi ya kukusanya ushuru kabla ya kulipa fedha yote ya dhamana.**
4. **Mfumo wa kielektroniki (POS) ndio utakaotumika kukusanyia ushuru na wakala atalamizimika kuwasilisha Halmashauri mapato yote aliyokusanya kwa kutumia POS kwa kipindi husika na baada ya hapo Halmashauri itawajibika kumlipa wakala kiasi kinachostahili, hivyo mwombaji (wakala) lazima aoneshe ni asilimia ngapi atastahili kulipwa ambayo haitakiwi kuzidi asilimia 80% ila inaweza kuwa pungufu ya asilimia 80% ya makusanyo yote.**
5. Mwombaji awasilishe kotesheni halisi na nakala mbili.
6. Kotesheni ijazwe vizuri, iwekwe kwenye bahasha iliyofungwa kwa Lakiri baada ya kujazwa na juu ya bahasha iandikwe kwa **HERUFI KUBWA KOTESHENI ILIYOOMBWA** bila kuwekwa alama yoyote ya kumtambulisha muombaji.
7. **Mwombaji asiwe mtumishi wa serikali/shirika la umma.**

CamScanner